



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA TUNDURU



Mtaa wa Kalanje

Simu Na. +255 (026) 80004

Nukushi Na. +255 (026) 80208

BaruaPepe: info@tundurudc.go.tz

S.L.P 275

TUNDURU,

TANGAZO LA KAZI YA UJENZI WA JENGO LA OPD NA MAABARA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU KWA MCHANGANUO WA KAZI ZIFUATAZO.

KAZI "A" JENGO LA OPD

- a) UJENZI WA MSINGI NA BOMA JENGO LA OPD
- b) UPAUAJI NA UEZEKAJI JENGO LA OPD
- c) UWEKAJI WA MIFUMO YA MAJI SAFI NA TAKA JENGO LA OPD
- d) UPAKAJI WA RANGI NA MAPAMBO JENGO LA OPD
- e) UWEKAJI WA SAKAFU NA MARUMARU JENGO LA OPD
- f) UWEKAJI WA MIFUMO YA UMEME JENGO LA OPD

KAZI "B" JENGO LA MAABARA

- g) UJENZI WA MSINGI NA BOMA JENGO LA MAABARA
- h) UPAUAJI NA UEZEKAJI JENGO LA MAABARA
- i) UWEKAJI WA MIFUMO YA MAJI SAFI NA TAKA JENGO LA MAABARA
- j) UPAKAJI WA RANGI NA MAPAMBO JENGO LA MAABARA
- k) UWEKAJI WA SAKAFU NA MARUMARU JENGO LA MAABARA
- l) UWEKAJI WA MIFUMO YA UMEME JENGO LA MAABARA

**DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
TUNDURU**


TAREHE: 06.04.2023

1. Halmashauri ya wilaya ya Tunduru imepata fedha toka serikali kuu kwa ajili ya ujenzi ulioainishwa hapo juu
2. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya Tunduru anawaalika **Mafundi** wenye uzoefu wa kufyatua tofali ujenzi wa majengo kutuma maombi kwaajili ya ujenzi ulioainishwa hapo juu
3. Mchakato wa upatikanaji wa **fundi** utafanyika kwa njia ya ushindani kwa kuzingatia sheria za manunuzi ya umma za mwaka 2011 na mabadiliko yake ya mwaka 2016.
4. Waombaji wenye nia ya kazi waandike barua ya kuomba kazi hii kwa mkurugenzi Mtendaji (W)
5. Kama kuna vielelezo vya uzoefu waweza ambatanisha itawapa nafasi kubwa ya kushinda ushindani wa kazi japo sio lazima
6. Kila mwombaji atapewa kazi moja tu ili kuongeza ufanisi na usimamizi wa kazi.
7. Michanganuo ya kila kazi inapatikana bure katika ofisi ya Manunuzi **chumba No.35**
8. Maombi yaelekezwe kwa mkurugenzi mtendaji kwa anwani iliyopo chini kabisa (foot note) na yapelekwe ofisi ya Manunuzi **chumba No.35** na mara utakapokabidhi maombi yako kumbuka kusiini
9. Mwisho wa kupokea maombi haya ni Tarehe 13/04/2023 saa tano kamili asubuhi.11.00AM (SAA 5.00)
10. Kila mwombaji ataomba kazi mojawapo ya zilizoainishwa kwenye tangazo **mfano:** .
Ninaomba kufanya kazi ya ujenzi wa msingi na boma jengo la OPD au ninaomba kufanya kazi ya upakaji rangi na mapambo jengo la Maabara

Zingatia

Maombi yatakayo chelewa, maombi yasiyo kamilika, maombi ambayo hayatakuwepo siku ya ufunguzi, hayatapokelewa na kuhusishwa na zoezi la uchambuzi wa kumpata fundi atakayefanya kazi aliyoomba.

Nasisitiza: uombaji wa kazi ufuata utaratibu ulioelekezwa kwene maelekezo No.6 na maelekezo ya No.8 ni mhimu sana kama hutaelewa fika ofisi ya Manunuzi utaelekezwa vizuri kabisa.



JECELYNE MGANGA

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)

TUNDURU

**DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
TUNDURU**